

PAZIA LA PILI

Hama kweli! Pozo la mtoto mtukutu maficho yake uvungu kukwepa viboko vya mzazi! Baada ya wanadamu kulala fofofo kwa usiku mzima wa giza utadhani walifukiwa kaburini kwa muda. Siku mpya ilianza na juu lilituma salaamu za miyonzi yenye nuru kali kuisalimu dunia, kuwa giza limetoweke na watu waanze kuendelea na shughuli zao za mchana. Ndege waliimba mitini kwa sauti zao walizoumbiwa na MUNGU, majogoo waliwika kokorikoo! Kokorikoo! juu ya mabanda yao wakitoa ishara ya mapambazuko, huku Ngo'ombe wakitoa milio yao MOO! MOO! Wakidai kupelekwa malishoni na wachungaji wao, bila kujali mbwa nao walibweka kwa viburi mithili ya kuwa wanafukuza wezi. Ndipo mwanaume mwenye hulka yake alianza kukatiza mtaa kwa mtaa huku macho yake yaliyojaa umakini utadhani mchimba dhahabu mgodini! Lakini cha

kumuacha mdomo wazi mitaani hakuona mtu yejote, palikuwa pametulia tuli kana kwamba hapakuwahi kuishi watu mahali pale, alizidi kusonga akikata kona hii na ile. Aliuona mti wa muembe na kisha aliusogelea na kukaa chini yake. Baada ya muda mti ulianza kuyumba yumba kana kwamba kuna upepo lakini alipoangalia hali ya hewa ilikuwa imetulia kabisa, hata miti jirani haikuyumba kabisa, aliendelea kukaa na kadri muda ulivyoenda mti ulikuwa kama kuna mtu anaukata na ulikuwa unaelekea kuangukia upande alioketi kijana huyu. Kwa haraka alinyanyuka na kuondoka, alipofika mbali aligeuka na kuangalia kilichotokea pale mitini lakini cha kushangaza mti ulikuwa umetulia tuli! "**Mmh!! ni Macho yangu!** ama kweli kila boriti na mwandamizi wake" kijana alinena kwa kinywa chake. Njaa nayo ilianza malalamishi yake ndani ya mahakama ya tumbo lake na kumsumbuu ili atimize marejesho ya haki ya shibe, ndipo akaanza kutahamaki huku na huku akiangalia huku na kule. Kwa mbali aliuona

MAREHEMU KUTUBU KABURINI

mchungwa na mpera, kwa haraka alipiga hatua ili akapate hata kutuliza njaa. Alianzia kwenye mchungwa kwani alikuwa na kiu sana, aliangua machungwa kama matano hivi na kisha aliketi **chini kwa kukunja miguu yake kwa mbele**, na akamenya chungwa la kwanza lililokuwa limeiva vizuri sana, hivyo alitegemea kupata maji maji ya kutosha lakini ilikuwa ajabu ndani ya chungwa palikuwa hakuna maji maji palinyaukiana sana, hivyo hakuweza kula lile chungwa, alichukuwa chungwa la pili, alilimenya lakini pia matokeo hayakuwa mazuri maana kwa ndani lilikuwa bichi kabisa na alilitupa. Kwa matumaini sana alichukuwa chungwa la tatu lilionekana kumvutia sana, akaanza kulimenya, kuangalia kwa ndani chungwa lilikuwa zuri sana, maji maji yalioneckana ya kutosha, mate yalimjaa kweli kweli **utadhani chopeko na mnofu**, baada ya kubugia lile chungwa alikunja sura kwani alikutana na ladha kama ya ndimu ndani ya chungwa lililoiva, alilitupa huku akijisemea "huu mti hauna maana kabisa" kwa hasira ya njaa alipukutisha nusu ya machungwa